



COUNTY ASSEMBLY OF MOMBASA

OFFICIAL REPORT

Thursday, 25th October, 2018

The House met at 2:46p.m.

(The Speaker (Hon. Aharub Ebrahim Khatri) in the Chair)

PRAYERS

The Speaker (Hon. Khatri): Hon. Members you may be seated. Yes Clerk?

STATEMENTS

RESPONSE TO STATEMENT BY CHAIRPERSON COMMITTEE ON TRANSPORT, INFRASTRUCTURE AND PUBLIC WORKS ON CLEANING OF DRAINAGE FROM MAGONGO MAINLAND TO AKAMBA HANDICRAFT

Yes Hon. Prischillah Mumba, the Chairperson Committee on Transport, Infrastructure and Public Works please give the statement response.

Hon. (Mrs.) Mumba: Thank you Mr. Speaker. Mr. Speaker sir I wish to give the following statement on cleaning of drainage from Magongo Mainland to Akamba Handicraft which was requested by Hon. Faith Mwende, MCA Kipevu Ward on Thursday, 16th August, 2018 during the 70th Sitting.

Mr. Speaker sir in the financial year 2017/2018 the County had contracted youth companies to work on drain cleaning in various zones including Mainland West (Changamwe sub zone).

The youth companies have not been paid for the work done for the last two quarters of the financial year, and due to that it has become quite difficult for the youth to continue working given that their capacities are limited.

The County and relevant Committees should ensure timely payment for such works for the programme to be sustained.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you Hon. Prischillah, yes Hon. Faith Mwende?

Hon. (Ms.) Mwende: Mheshimiwa Spika sija ridhishwa na majibu ambayo yametoka kwa kitengo cha Uchukuzi na Miundo Misingi nikikumbuka vizuri nimekaa pale tangu utoto wangu na huo mtaro ambao tunauzungumzia kutoka Mainland mpaka Akamba Handicraft hakujawahi kuwa na vijana wowote! Ilipata nusra kidogo wakati kulikuwa na vijana ambao walijitolea kutoka National Youth Service (NYS) kuja kusafisha na huo mtaro ndio unabeba maji yote yenye yanatoka Airport na Portreitz na saa hii tunaongea Mheshimiwa Spika, saa hii kuna vita vinaendelea pale tangu asubuhi nimeshinda kupiga simu na hakuna lolote linafanyika. Mheshimiwa Spika hili si jambo la leo wala jana, hili ni jambo mwenyewe hususan nilienda kwa kitengo nikawaeleza shida hizi lakini mpaka saa hii hakuna hatua ambayo imechukuliwa na hata kama wanalalama hakuna pesa kile kidogo ambacho bajeti wamepitisha wameweza kuifanyia nini mpaka siku hii ya leo. Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you Hon. Faith. Hon. Prischillah Mumba I think the best thing you can do is maybe the Committee of Transport and Infrastructure if they can visit that place and maybe you can come up with a relevant solution so that you can sit down with CEC Member and know if the problem has been solved or not yet, thank you. Yes Clerk?

RESPONSE TO STATEMENT BY CHAIRPERSON COMMITTEE ON TRANSPORT, INFRASTRUCTURE
AND PUBLIC WORKS ON THE INSTALLATION OF DIGITAL HIGH MAST STREET LIGHTS IN DENSELY
POPULATED AREAS

Yes again Hon. Prischillah Mumba? please give the response of the statement

Hon. (Mrs.) Mumba: Thank you Mr. Speaker. Mr. Speaker sir I wish to give the following statement on Installation of digital high mast street lights in densely populated areas which was requested by Hon. Charles Kitula Frere Town Ward on Thursday, 27th September, 2018 during the 75th Sitting.

Mr. Speaker sir during the implementation of the 2017/18 financial year budget, the County failed to allocate monies for streetlights. This was however corrected when the money was allocated with the supplementary budget and works started in June, 2018.

Currently the department is repairing all existing street lights and high mast lights so as to have them functional. Upon the completion of this exercise then the installation of addition lights will be considered as per the needs of respective Wards.

The Department has planned site visits to all Wards and will give recommendations on improvement of lighting across Mombasa County. A schedule works and summary executed in the 1st quarter of 2018/2019 in each Ward as attached.

We had no maintenance materials for more than one year. Fortunately, we received some materials in June which we had three programs cycles as per attachments...

(Interruption)

The Speaker (Hon. Khatri): Hon. Prischillah I think this document was here last week, you were reading this paper and you brought it again the same paper?

Hon. (Mrs.) Mumba: Yeah because it is the reply of this statement.

The Speaker (Hon. Khatri): Yes you may continue.

Hon. (Mrs.) Mumba: ... as per attachments.

The list of items allocated for each Ward is as follows;

Phase one was 20 pieces Hps 150w bulbs, 10 pieces of 150w ballast, 5 pieces 70-400w ignitors, 3 pieces 250w ballast, 2 pieces 50 Amps 2 Pole contactor, 1 pieces timer switch, 5 pieces circuit breaker and two is phase two which is 16th July...

(Interruption)

The Speaker (Hon. Khatri): Hon. Prischillah so this is phase one and each Ward received these items?

Hon. (Mrs.) Mumba: Yeah.

The Speaker (Hon. Khatri): ...and did you give this copy to each Member? Did you give the copies to the Members?

Hon. Members: No!

The Speaker (Hon. Khatri): So the Members should have the copies so that they can confirm. Clerk, is there anyone with this copy, the one with the phases?

Hon. Members: We don't have!

The Speaker (Hon. Khatri): No one has that copy Clerk! So how will the Members even confirm if they have ever seen these things in the Ward? Yes you can continue Hon. Prischillah, I think you have already read phase one which is between 18th June to 12th of July, yeah?

Hon. (Mrs.) Mumba: Yes, we have phase two which was 16th July to 10th August 20 pieces...

(Interruption)

The Speaker (Hon. Khatri):...and this again it is in each Ward.

Hon. (Mrs.) Mumba: Yeah!

The Speaker (Hon. Khatri): You are saying each Ward have receive these things?

Hon. (Mrs.) Mumba: Phase one was the first one and this is phase two, now am reading;

Phase two was also 20 Pieces 150w bulbs, 7 pieces...

(Interruption)

The Speaker (Hon. Khatri): Hon. Ibrahim Omondi?

Hon. Omondi: Thank you Mr. Speaker. I would like to inform the House on this same issue that Hon. Prischillah Mumba is reading. Mr. Speaker sir I thought that it could be wise if the Chairperson could organise for the copies so maybe in the next sitting so that the Members should have the copies for the confirmation because even if they read Mr. Speaker it doesn't help us at all, we cannot be able to take all that materials that is reading Mr. Speaker sir. Thank you.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you, yes Hon. Maimuna?

Hon. (Ms.) Maimuna Salim: Mheshimiwa Spika nashukuru kwa kunipatia fursa hii. Mimi yangu ni masikitiko kwa Waheshimiwa wenzangu ambao wamesimama kwa sababu Mheshimiwa Prischillah yeye anapewa ripoti, kwa hiyo hiyo si kazi yake ni kazi za Makarani wa Bunge ambao ndio wapatiane ripoti. Kama tunavyoingia tukichukua *order paper* ilikuwa tuchukue pale; mimi sioni inayotendeka ni haki kwa upande wa Mheshimiwa Prischillah kulingana na hizi zinazoendelea hapa wanaume ni kama ambao wanataka kuleta hujuma kwa huyu Mheshimiwa mama na sisi hatutokubali...

(Applause)

The Speaker (Hon. Khatri): *Hon. Maimuna hizo fikra zenu sijui munatoa wapi? mimi sioni kama hapa kuna anything personal, you know there's nothing personal. Hon. Maimuna to be honest this thing is not personal and even the last time if I remember I told Hon. Prischillah that Committee you are sitting on has so many things so don't take it personal when people are here to talk about these issues, they have problems in their Wards so please Hon. (??) and this thing about the photocopies the problem is not about Hon. Prischillah if you can hear I told the Clerks...I didn't say Hon. Prischillah where are the copies? I instructed the Clerks, where are the copies? So let us not change the topic, yes you can continue Hon. Prischillah and Hon. Members will have the copies I think. Clerk, make sure all the Hon. Members have the copies now please? Yes Continue with phase two Hon. Prischillah Mumba.*

Hon. (Mrs.) Mumba: Thank you Mr. Speaker for defending me on that matter. If I may continue reading the statement as I had started phase two am repeating;

Phase two that was 16th July to 10th August 20 Pieces 150w bulbs, 7 pieces 150w ballast, 15 pieces 70-400w ignitors, 3 pieces 250w Hps bulbs, 2 pieces 250w ballast, 2 pieces 50 Amps 2 pole contactor and 1 piece timer switch, 5 pieces circuit breaker that was phase two and then we go to phase three that was done on 19th September to 16th October which was 15 pieces Hps 150w, 2 pieces 70-400w ignitors and 3 pieces circuit break.

These were the challenges which they indicated;

Lack of enough maintenance materials, lack of technicians, lack of working and safety gears, lack of continuous working status of street lighting fleet.

Thank you Mr. Speaker.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you Hon. Prischillah Mumba.

(Applause)

Yes Hon. Charles Kitula?

Chief Whip (Hon. Kitula): Mheshimiwa Spika nimesimama kwanza kumpatia kongole Mwenyekiti wa Kamati ya Uchukuzi....

(Applause)

Kwa juhudi anazozifanya Mheshimiwa Spika kuhakikisha kwamba analeta ripoti katika Bunge hili lakini vile vile ningependa iwe kwenye kumbukumbu kwamba shida hii ya taa za barabarani ni donda sugu katika Kaunti ya Mombasa na shida si Mwenyekiti huyu Mwenyekiti anaomba taarifa kutoka Idara ya Uchukuzi anapoandikiwa pale inakuja moja kwa moja hapa na ni dhahiri shahiri kuwa hakuna Waziri, hakuna Afisa Mkuu ambaye ataleta taarifa ambayo itampiga mwenyewe au kusema kwamba hajafanya kitu fulani. Tusidanganyane Waheshimiwa wenzangu kila Mbunge, kila Waziri na kila Afisa Mkuu ataandika taarifa kwamba hili linaendelea mashinani lakini ni ukweli jamani sisi ndio wabunge tunaowakilisha kila sehemu, suala la masuala ya mataa Mheshimiwa Spika limekuwa donda sugu sana....

(Applause)

Shida Mheshimiwa Spika huenda ikawa sio Waziri, shida huenda isiwe sio *Chief Officer*, shida huenda sio *Procurement officer* saa hizi tumeambiwa kwamba 20 *pieces* kwa kila Wodi mimi ningependelea kama kiranja wa Bunge hili kupitia maoni haya ambayo idara imeweza kutuletea na pia tungependa maoni ya *procurement* waweze kutuletea barua kwamba wakati wa Juni na Julai 2017 wali *procure* vitu vingapi? Watuletee halafu tulinganishe na hii ndio tujue kweli hivi ni vitu vinakuwa *procured* au la ni stori tu kitengo inatuandikia ili kuweza kutufurahisha sisi Bungeni. Ahsante sana.

(Applause)

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you Hon. Charles Kitula. The Chairman of Finance I think is not here, any other Member of Finance maybe...?

(Hon. (Mrs.) Prischillah Mumba stood up)

You are also a Member so you can check with your Finance team what Hon. Charles Kitula is asking about.

If these things were really procured then you can bring the answer maybe next week on that list, okay Hon. Prischillah please next week Thursday if you can bring the answer. Yes Clerk?

RESPONSE TO STATEMENT BY CHAIRPERSON TRANSPORT, INFRASTRUCTURE AND PUBLIC WORKS
ON GRADING AND GRAVELLING OF MWAKIRUNGE ROAD LEADING TO MWAKIRUNGE DUMPSITE

The Speaker (Hon. Khatri): Yes again Hon. Prischillah Mumba kindly give the response?

Hon. (Mrs.) Mumba: Thank you Mr. Speaker. Once again Mr. Speaker I wish to give the following statement on grading and gravelling of Mwakirunge Road leading to the dumpsite which was requested by Hon. Feddis Salame MCA Mwakirunge Ward on Thursday 27th September, 2018 during the 75th Sitting.

Mr. Speaker sir, the road in question is classified as a national road and under the management of both Kenya Urban Roads Authority (KURA) and the Kenya Rural Roads Authority (KERRA).

The road is currently being maintained by KURA and KERRA hence the County cannot utilize her funds on the same as this will attract audit queries. Furthermore the road requires huge amounts of money for improvement hence should be budgeted for adequately if the County has to do it due to the interest in the dumpsite.

Thank you Mr. Speaker.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you Hon. Prischillah Mumba, yes Hon. Feddis?

Hon. (Mrs.) Mbura: Ahsante sana Mheshimiwa Spika na pia nampongeza mamangu mpendwa Mheshimiwa Prischillah kwa hiyo ripoti lakini barabara ninayolilia si barabara ya serikali kuu ile kubwa ni kwamba Kaunti kama itawezekana waweze kutoa kuanzia ile barabara ya serikali kuu kuingia ndani ili wakati gari zikipeleka taka ziingie ndani zipeleke taka mahali kunatakikana kwa sababu saa hii kusema kweli Mheshimiwa Spika barabara yote imezibwa. Kama kungekuwa na barabara ya *murrum* ya kuingia ndani kulikuwa na jaa hatungekuwa na hiyo shida, hivyo basi hivyo ningepomba tu niweze kupata tena majibu kama Kaunti inaweza kupeana hiyo barabara kuanzia mwisho wa ile barabara ya *national* mpaka ndani. Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you Hon. Feddis Salame. Yes Kitula, Hon. Kitula?

Chief Whip (Hon. Kitula): Mheshimiwa Mwenyekiti kusema kweli mimi nishawahi kuzuru katika Wodi ya Mwakirunge; hili tatizo limekuja sana Bungeni katika kumbukumbu zetu hivyo basi tungependa sana Mheshimiwa Mwenyekiti leo hii toa uamuzi ndani ya wiki tatu au ndani ya mwezi mmoja barabara ile itengenezwe maanake lori zetu zote za Kaunti zinaenda Mwakirunge. Mheshimiwa Mwenyekiti sasa hivi ukisema kuwa hii taarifa irudi kwa idara itakuwa tunamuonyesha unyonge Mheshimiwa Mwenyekiti Mheshimiwa wa Mwakirunge.

Malori yote yanakwenda Mwakirunge na barabara kule ni mbovu hasa wakati huu wa barabara ikiwa takataka zile zinamwagwa barabarani yataonekana vipi katika Bunge letu Mheshimiwa Mwenyekiti.

(Applause)

Kwa hivyo leo tuo uamuzi Mheshimiwa mwenyekiti tumsaidie tutoe kama ni mwezi mmoja barabara iwe inatengezwa na kama haitatengezwa sisi kama Bunge tuweze kuchukua uamuzi Mheshimiwa Mwenyekiti. Ahsante sana.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you Hon. Kitula. Yes Hon. Lucy Chizi?

Hon. (Ms.) Chireri: Ahsante sana Mheshimiwa Spika mimi ninaunga mkono Mheshimiwa Feddies, Mheshimiwa Kitula. Mheshimiwa Spika hali ilioko Mwakirunge sasa hivi ni hali ngumu sana; kwanza huu msimu wa mvua ambao uko hakuna barabara, takataka zinamwaywa hiyo barabara. Pikipiki zinatafuta mahali, kama pikipiki itatafuta mahali wewe binadamu utaenda wapi? Mheshimiwa Spika kuna dharura sana, Mwakirunge ni Kaunti ya Mombasa kwa hivyo nayo inataka kutengenezwa, takataka zote sasa za Mombasa nzima zimeenda Mwakirunge. Kama takataka Mheshimiwa zaenda kule pia wa Mwakirunge nao wanataka waangaliwe; barabara, hospitali kila kitu mwanzo tumewapelekea magonjwa kule iko haja ya dharura leo hii tunasema barabara lakini kipindupindu kiko tele kule, watoto wanaumwa na maumbwa usiku wanapotafuta chakula kule, Mwakirunge iko haja ya kuangaliwa kiundani vilivyo na hii ni dharura. Tunaita janga la Kaunti ya Mombasa hiyo Mwakirunge Mheshimiwa Spika kwa hivyo ninaomba iangaliwe kwa jicho la huruma sio tumuangalie eti ni Mheshimiwa Feddies tunaangalia wa Mwakirunge wote wako katika hali mbaya. Ahsante Mheshimiwa Spika.

The Speaker (Hon. Khatri): Ahsante sana Mheshimiwa. Yes Hon. Ahamed Salama.

Hon. Ahmed Salama: Ahsante Mheshimiwa Spika siku zile niliposema hapa Mwakirunge yatisha ni kama si Mombasa; Mheshimiwa wa kule alilalamika sana lakini kusema ile ukweli Mwakirunge imekaa kama ambaye si Mombasa, kwa hivyo tunaomba hili swala hili lishughulikiwe haraka kwa sababu yatisha sana Mwakirunge. Ahsante.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you, yes Honourable.

(Some Members stood)

Relax Hon. Members! Just relax I will call you by your names. Just relax, sit down Hon. Members, relax! Ahmed Salama, you have finished?

(Hon. Ahmed Salama nodded in the affirmative)

Okay, Hon. Faith please?

Hon. (Ms.) Mwende: Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Ninashukuru Mwenyekiti wa Uchukuzi kwa kuwajibika kwa wakati ambao unaofaa hilo mpaka tumpatie kongole...

(Applause)

Mheshimiwa Spika tukiongelea hali ya Mwakirunge mimi nimeenda mikutano mingi na kina mama wa Mwakirunge nikasikia kilio chao; unapata pale sehemu ya takataka mama hata anaanguka anaangukia mabuu, mwengine ilikuwa hali ya kusikitisha tuko pale kama

Wabunge mama anasema zingine hata ziliingia kwenye mdomo. Hali ile ya pale ni mbaya sana na Mheshimiwa Spika si njia ya idara ya uchukuzi kuhepa majukumu kama ile barabara kuu ni ya serikali kuu. Kuna hicho kichocho chenye Mheshimiwa aliongelelea hususan yenye inapeleka takataka, hivyo basi Mheshimiwa Spika si mambo hapa ya kubembelezana ama kuogopana ni utenda kazi ufanyike kwa vile mwisho wa siku sisi Waheshimiwa ni sisi tunalaumiwa. Waziri wa Uchukuzi na watu wale wake wote wanafanya kazi, hili jambo lichukulie la dharura sana tena sana. Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you Honorable. Yes Hon. Bwire?

Hon. Bwire: Shukran Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika mjadala ni mzuri ila nataka tukumbushane ya kwamba tunapojadiliana pia tukumbuke ya kwamba idara ya mazingira nayo inafaa ihusishwe katika mchakato mzima wa lile swala. Kwa hivyo ningeliomba Mwenyekiti wa Kamati ya Mazingira washirikiane na Mwenyekiti wa Kamati ya Uchukuzi tunapozungumzia kuhusu kumwaga takataka tunazungumzia idara ya mazingira. Sasa hapa ni kwamba idara ya Uchukuzi iangalie njia jinsi gani magari yatapita yasimwage takataka pale na hawa idara ya mazingira wasimwage taka kusudi barabarani kwa sababu hawataki kuingia ndani. Kwa hivyo hizi idara mbili Mheshimiwa Spika ni ombi langu ya kwamba washirikiane kwa pamoja kusaidia watu wa Mwakirunge. Ahsante.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you, yes Hon. Thoya.

Hon. Thoya: Ahsante sana Bwana Spika. Mimi nafikiri swala hili la Mwakirunge kufikia saa hii hata wakati tunajaribu kulipeleka kwa Kamati ya Uchukuzi ni kama ambaye tunazidi kutesana lakini limefika kwamba ni swala la...*(Technical hitch)* ingewezekana Bwana Spika ungelitilia uzito na ukatambua ipo haja Jumba hili lote likiongozwa na wewe mwenyewe Spika tuweze kutembea Mwakirunge kuweza kujionea na macho ama mimi naona tukizidi kulisukuma kwa Mheshimiwa Priscilla na Mheshimiwa Kitula...

(Interruption)

The Speaker (Hon. Khatri): Yes Hon. Thoya you can continue.

Hon. Thoya: Nilikuwa nataka uyasikie vilivyo haya.

The Speaker (Hon. Khatri): Ndio nayasikia twende Mwakirunge na kusikiza.

Hon. Thoya: Naomba Jumba hili liweze kupata safari; safari hii twendeni Mwakirunge tusiende Nairobi wala Kilifi twendeni hapa hapa tukajionee kwa sababu shida haianzi. Hii alikuja akasema wazi hapa wasichana wake saa hii wanabakwa na kasha kwa maji nafikiri yalienda hivyo hivyo; ikaja sasa ni mambo ya barabara takataka zinamwagwa sijui ingekuwa ni vyema wale watu wa Mwakirunge saa hii wakasema kwamba sasa hizi takataka nazo zisije huku Mwakirunge nyinyi mtasema nini?

Kwa hivyo nataka kumshukuru Mheshimiwa Feddies kwamba hawatii sumu watu wake lakini ikiwa ni lazima mlete taka nyinyi nanyi jukumikieni hizi barabara zetu. Wakesema kwamba hizi barabara kama hazitatengezwa takataka nanyi kila mmoja amwage kwake mtasemaje? Kwa hivyo naomba Bwana Mwenyekiti na ikiwa ni Wodi ambayo inataka kukuzwa basi ni Wodi ya Mwakirunge na zingekuwa pesa ziko kungekuwa na kama vile

wazungu wanasema *equalization funds* Mwakirunge ingeweza kupelekewa pesa za kutosha ili ifikie Wodi zingine ambazo kwa saa hii zinang'ara. Bwana...

(Interruption)

...Mbona mnanitesa!

The Speaker (Hon. Khatri): Yes, *endelea Hon.Thoya nakusikiza.*

Hon. Thoya: Mimi nimemaliza nimesema hata wakati tunapanga hizi pesa tuiangalie kwamba Mwakirunge ndio Wodi kitinda mimba ambayo inahitaji kukuzwa iwe sawa sawa na Wodi zingine lakini pale yalipofikia Bwana Spika si ya Mheshimiwa Priscilla pekee yake. Ngingekuomba wewe mwenyewe itatia moyo sana wale watu wa Mwakirunge waone kwamba Spika na Nyumba nzima imetembelea pale, itasema kweli sisi tunawajali sana. Ahsante.

The Speaker (Hon. Khatri): Ahsante Mheshimiwa Thoya na nafikiri ni muhimu kupanga hilo jambo kwa hivyo Mungu akipenda wiki ijayo tutapanga. Yes Hon. Kitula?

Chief Whip (Hon. Kitula): Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante kunipatia fursa hii na vile vile ni kuongezea pale kwa Mheshimiwa Thoya ametoa wazo zuri sana kwamba sisi Wabunge sote tuweze kuandamana hadi kule sehemu ya Mwakirunge lakini vilevile Mheshimiwa Mwenyekiti pia mimi nina wazo kwa hapo hapo katika Mheshimiwa Thoya alipoongelea sisi ndio tutaenda pale kama Wabunge lakini tupate kuifahamu pia kwamba watenda kazi ni hawa *executive* Mheshimiwa Thoya. Kwa hivyo ni bora zaidi mimi ningeona kwamba kabla hatujaweza kufika kule kama Wabunge waje hapa katika Bunge letu tuandaamane na wao wenyewe hadi Mwakirunge uamuzi utolewe palepale sisi tukiwa na wao wakiwa pale...

(Applause)

Kwa hivyo waje Bungeni hapa tuweze kuzungumza mambo yetu wenyewe kwa wenyewe halafu tuandamane na wao mpaka Mwakirunge Mheshimiwa Mwenyekiti. Ahsante.

The Speaker (Hon. Khatri): Mheshimiwa Priscilla shida nyingi naona ziko upande wa uchukuzi hapa; nikiangalia kila mmoja kilio chake analia ni upande wa uchukuzi kwa hivyo mtaangalia vile upande wenu kama maanake Waheshimiwa kila unapopeana jibu naona hawaridhiki hivyo pengine labda umuite huyo Waziri wa Uchukuzi aje hapo na Waheshimiwa mkae kwenye Kamati ajibu hayo maswali kama kutasaidika mjue. Sio kila siku ni tunakaa *response* peleka, jibu peleka, jibu peleka na hakuna kitu kinafanyika, kwa hivyo mwangalie kama Kamati mko na nguvu za kumuita mkubwa wa kitengo hicho. Kama ni kumuita muiteni huyo Waziri ama ni kama ni afisa mkuu waje, waheshimiwa wako hapa kuwakilisha wananchi na wananchi wanashida na kama wananchi hawasaidiki sasa kuna faida gani? *Thank you. Yes Clerk?*

RESPONSE TO STATEMENT BY CHAIRPERSON YOUTH, GENDER, SPORTS AND CULTURAL AFFAIRS
ON COUNTY GOVERNMENT PLANS TO AWARD COUNTY EMPLOYEES IN NATIONAL SPORTS
COMPETITIONS AS A WAY OF MOTIVATING THEM

Yes Hon. Aran Moses please give the statement?

Hon. Aran: Thank you Mr. Speaker. Mr. Speaker I wish to give the following statement on awarding County employees in national sports competition in response to concerns raised by Hon. Fadhili Mwalimu in the House on the 75th Sitting seeking to know from the Committee on Youth, Gender, Sports and Cultural Affairs whether Members are aware that some County employees have been posting tremendous results in national sports scooping awards in different categories and whether the County government has any plans to reward such employees as a way of motivating them.

Mr. Speaker sir the Department recognizes the need to motivate both individual and employee teams that exemplary achieve outstanding performance in national and international competitions. In this regard they intend to include the modalities to award achievers in the planned sports policy by the Department.

Mr. Speaker sir the department shall therefore consult with the Department of Devolution and Public service before coming up with final recommendation.

Thank you Mr. Speaker sir.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you Hon. Moses Aran. Yes Clerk?

RESPONSE TO STATEMENT BY CHAIRPERSON OF IMPLEMENTATION COMMITTEE ON
IMPLEMENTATION STATUS OF MOTIONS PASSED IN THE HOUSE SINCE INCEPTION OF THE SECOND
ASSEMBLY

Yes Hon. Salim Kalume?

Hon. Salim Kalume: Thank you Mr. Speaker sir. Mr. Speaker sir I am standing in regards to a statement requested by Hon. Mohamed Hatimy on the implementation of Motions passed in the House since inception of the Second Assembly on Thursday 4th October, 2018 during the 75th Sitting. Mr. Speaker sir first allow me to bring to the attention of the House that I was not given 21 days as it was stated by Hon. Speaker during the 85th sitting on Thursday 18th October, 2018 at 2:30p.m. Instead Mr. Speaker sir I was given 14 days to the response, this can be confirmed in the Votes and Proceedings and the Hansard records. Mr. Speaker sir the Committee on Implementation has managed...

(Interruption)

The Speaker (Hon. Khatri): Hon. Salim Kalume, who gave you 14 days?

Hon. Salim Kalume: You gave me 14 days.

The Speaker (Hon. Khatri): You asked for 21 days, three weeks?

Hon. Salim Kalume: Yes?

The Speaker (Hon. Khatri): And I gave you three weeks.

Hon. Salim Kalume: No you gave me two weeks.

The Speaker (Hon. Khatri): No but I agreed with you, if I remember I told you three weeks.

Hon. Salim Kalume: No the Hansard is there Mr. Speaker sir.

The Speaker (Hon. Khatri): You asked for one month, isn't it?

Hon. Salim Kalume: I asked for 21 days.

The Speaker (Hon. Khatri): Okay.

Hon. Salim Kalume: Yes and you gave me 14 days.

The Speaker (Hon. Khatri): Okay, alright continue?

Hon. Salim Kalume: Mr. Speaker sir the Committee on Implementation has managed to prepare a Motion tracker...

(Interruption)

The Speaker (Hon. Khatri): Because if you can read your statement very clearly, 'Mr. Speaker sir, first allow me to bring to attention to this House that I was not given 21 days as it was stated by Hon. Speaker'. So you are contradicting yourself, you are saying I have stated that you are given 21 days and now you are saying I have not given you 21 days so...

(Interruption)

Hon. Salim Kalume: No that is a little mistake, it was 14 days.

The Speaker (Hon. Khatri): Yes.

Hon. Salim Kalume: It was 14 days.

The Speaker (Hon. Khatri): Sorry it was...

(Interruption)

Hon. Salim Kalume: You gave me 14 days.

The Speaker (Hon. Khatri): So then why are you saying it was stated 21 days?

Hon. Salim Kalume: It is a clerical error Mr. Speaker sir.

(Silence)

(Table Clerk consultations)

The Speaker (Hon. Khatri): Yes Hon. Salim Kalume you may continue.

Hon. Salim Kalume: Thank you Mr. Speaker sir. Mr. Speaker sir the Committee on Implementation has managed to prepare a Motion tracker as attached. The House has

DISCLAIMER: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

Page 11

resolved 28 substantive and 41 Procedural Motions. Mr. Speaker sir, after the request of this statement, the Committee on Implementation resolved immediately to invite the County Secretary to a Committee meeting on the concerns that were raised by the Honorable Members. Mr. Speaker sir, the Committee managed to engage the County Secretary on the subject and after lengthy deliberations it was resolved that the County Secretary will make a follow up with concerned departments and report back to the Committee...

(Interruption)

The Speaker (Hon. Khatri): Yes Hon. Salim Kalume just hold on, yes Hon. Fadhili?

(Laughter)

The Deputy Speaker (Hon. Mwalimu): Thank Mr. Chair. Mr. Chair the Chairman for Implementation is presenting his response; he has said that there is a Motion tracker attached to this statement that is giving but unfortunately Mr. Speaker there is no tracker with us. Mr. Speaker i don't know where is the tracker?

The Speaker (Hon. Khatri): Clerks do you have the Motion tracker?

Hon. Salim Kalume: Yes I have.

The Speaker (Hon. Khatri): No Clerks! Clerks? You have the copies?

(Table clerks responded in the affirmative)

So you didn't share with the Members?

(Silence)

Yes you may continue Salim Kalume?

Hon. Salim Kalume: Mr. Speaker sir, in regards to the aforementioned the Committee would wish to seek for three more weeks to enable the office of the County Secretary and...

(Interruption)

The Speaker (Hon. Khatri): Yes Hon. Mohamed Hatimy?

Hon. Mohamed Hatimy: Mheshimiwa Spika hatuna *copies*.

The Speaker (Hon. Khatri): Clerks can you please do your work and give the copies to the Members...

(Loud Consultations)

So you are telling me that there is no enough papers in the House?

(Silence)

So the Clerks are saying that there are no enough papers in the House so there is a problem with the procurement, is that what you are saying?

(Silence)

Yes you can continue Hon. Salim Kalume.

Hon. Salim Kalume: Mr. Speaker sir, in regards to...

(Interruption)

The Speaker (Hon. Khatri): Yes Hon. Fadhili?

The Deputy Speaker (Hon. Mwalimu): Thank you Mr. Speaker. Mr Speaker to add on the Hon. Member is not properly dressed...

(Laughter and applause)

The Speaker (Hon. Khatri): Hon. Fadhili I think I can see him he is properly dressed. I do not know I am blind here can you tell us what is that he is not properly dressed?

The Deputy Speaker (Hon. Mwalimu): Mr. Speaker I am wondering why the Serjeant left him to come in this Assembly with slippers and jeans...

(Laughter)

The Speaker (Hon. Khatri): Hon. Salim Kalume is it true that you are wearing slippers?

Hon. Salim Kalume: Mheshimiwa Spika nafikiri sote twajua kwamba huu ni msimu wa mvua na leo mvua imekesha na kwangu nyumbani nimevujiwa na nguo zote karibu zimetota, kwa hiyo namjibu Mheshimiwa Fadhili kwamba sikupenda kwangu kuja na *jeans* lakini ni kwa sababu ya ile hali ilioko katika Kaunti ya Mombasa.

(Applause)

The Speaker (Hon. Khatri): But Hon. Salim Kalume you know this House has procedures to be followed.

Hon. Salim Kalume: Nakubali.

The Speaker (Hon. Khatri): You cannot just ... Sergeant-At-Arms ...you know... Hon. Sergeant-At-Arms at least you should advise the House at least we know what is going on. You should do your work. Yes Hon. Kitula?

Chief Whip (Hon. Kitula): Mheshimiwa Spika nafikiri japo kuna nidhamu ya Bunge lakini Waheshimiwa wenzangu wanarifhamisha kwamba hatuendi sawa kama Bunge; endapo Mheshimiwa atatolewa ni bora pia basi ile ripoti mwana Kamati yeyote aweze

kuisoma ili Mheshimiwa Hatimy na Bunge hili liweze kupata ripoti kwa muda ulioweza kukezwa na Bunge Mheshimiwa Mwenyekiti.

The Speaker (Hon. Khatri): I think the Hon. Member stated very clearly that he had his issues and it is raining and all the Members know that it is raining so for now we can exempt him so that he may continue because from up I can see he is well dressed but Serjeant-At-Arms at least keep an eye this is your job we do not have to keep on telling you what to do. Yes you may continue Hon. Salim Kalume?

Hon. Salim Kalume: Ahsante Mheshimiwa Spika kwa kunilinda.

Mr. Speaker sir, in regards to the aforementioned the Committee would wish to seek for three more weeks to enable the office of the County Secretary and the Committee to collect tangible information to table in this Honourable House.

Mr. Speaker sir the Committee is not only interested in the status of implementation but also reasons to why some Motions are not fully or yet to be implemented. Mr. Speaker sir, going forward I want to assure this House the Committee on Implementation is committed to its course as expected of it as per the Standing order 189.

Thank you Mr. Speaker sir.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you Hon. Salim Kalume...

(Applause)

Yes Hon. Mohamed Mohamed Mohamed...

(Silence)

Yes Hon. Mohamed Mohamed Mohamed.

Hon. Mohamed Hatimy: Ametupatia *tracker* ambayo inasema uwongo.

The Speaker (Hon. Khatri): Yes.

Hon. Mohamed Hatimy: Tracker yasema uwongo, Miswada mingi imeandikwa *adopted, adopted adopted* na hatujui anamaanisha kitu gani.

Kwa hivyo hii stakabadhi haiko sawa, sijui *adopted* inamaanisha kitu gani Mheshimiwa Spika, *adopted* inamaanisha kuwa yataka... ikiwa ni *adopted* kitu kishafanyika kije na ripoti yake kuwa hiki kitu kimefanyika na hakuna ripoti yoyote na kusema kuwa wanauliza kutaka wiki tatu nyengine nafikiri huu umekuwa mchezo sasa. Hii ni kwa sababu Mswada kuna kitabu pale ambacho tukitoka kwenye hii Nyumba na nyinyi pia mko na *Vote Book* yenu yaonyesha leo sisi tumefanya nini; kitu ya kuonyesha kuwa *adopted* ni kuwa kupatikana ripoti ya kusema hii kitu tayari imekuwa *adopted* lakini vitu vyote hivi Mheshimiwa Spika ni ripoti ya uwongo hivyo basi hii nataka itupiliwe mbali kwenye hili Bunge.

The Speaker (Hon. Khatri): Yes Hon. Thoya.

Hon. Thoya: Mheshimiwa Spika pia mimi ni mwanachama wa Kamati hii ya Utekelezaji na kama siku hiyo ilipotafutwa ripoti hii nilisema sisi bado ni wanagenzi na hata nikatatizika na kitu inaitwa *Motion tracker*. Nashukuru siku hiyo kabla ya kwenda mafundisho niliweza kuipata na nikajua ni nini; tunaweza kujaribu na tukapata hayo lakini ukiangalia aya ya mwisho Mwenyekiti amesema, '*Mr. Speaker, going forward I want to assure this House the Committee on Implementation is committed to its course as expected*', na tutajaribu kuhakikisha zile ambazo zimepitishwa hapa je, *executive* inatekeleza? Kwa hivyo ningeomba tuzidi kupewa muda mwafaka kuangalia zile ambazo zimepitishwa hapa na zimeenda mpaka kwa *executive* kwa sababu si hizi peke yake, ziko nyingi ambazo zilipitishwa mwaka jana ambazo bado tunazitafuta ili kujua je *executive* inatekeleza na nafikiri Katibu wa Kaunti kama alivyotumbaia alitumbia tumpatie kama wiki mbili zile zingine ili kuona kwamba je, kuna kitu kinatekelezwa na *executive*?

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you Hon. Thoya. Hon. Members if you can read the response of Hon. Kalume it was very clear that he was asking for another 14 working days so he said 14 working days; that means it is like three weeks Hon. Salim Kalume right? Because it's Monday to Friday working days so you have asked for working 14 days which is three weeks to enable the office of the County Secretary to reply. So we are going to give you that three weeks; I think you have heard Hon. Mohamed Mohamed claiming that whatever report you brought is not a genuine report, is it something that you have drafted yourself without the knowledge of the Clerks and other Members of this House? So please we are giving you three weeks, go and make sure you get a report, a clear report from the County Secretary and even bring us the proper Motion tracker which is going to be approved by the Clerk himself, make sure the Clerk stamps himself to approve that its the proper copy of the true original and make sure all Hon. Members have the copy the next time you are here which is three weeks from now then we can take it from there. Thank you Mr. Salim Kalume.

Hon. Salim Kalume: Thank you Mr. Speaker sir.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you, yes Clerk.

RESPONSE ON STATEMENT BY CHAIRPERSON COMMITTEE OF TRANSPORT, INFRASTRUCTURE
AND PUBLIC WORKS ON THE STATUS OF THE ROAD FROM JUNDA DISPENSARY TO JUNDA
NG'OMBENI AND JUNDA MISSION

Yes Hon. Prishcilla Mumba I can see again you have a response.

Hon. (Mrs.) Mumba: Thank you Mr. Speaker. Mr. Speaker sir, I wish to give the following statement on status of the road from Junda Dispensary to Junda Ng'ombeni and Junda Mission which was requested by Hon. Raphael Bwire MCA Junda Ward on Thursday, 23rd August, 2018 during the 71st Sitting.

Mr. Speaker sir, the road is planned for improvement in the financial year 2018/2019 which is yet to take place. This financial year the County has not procured any road works as the process of biennial tendering is ongoing.

However Mr. Speaker, the Department is going to undertake remedial works to enable residents access their homes. A site visit has already been done by the Director of

Roads and the area MCA. The road requires more funds as opposed to the current allocation.

Thank you Mr. Speaker.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you Hon. Pricilla Mumba, yes Hon. Bwire.

Hon. Bwire: Thank you Mr. Speaker. Mr. Speaker I stand to confirm that we did two site visits; that is after writing to the Department concerned and I also happen to serve your office with a copy as well as the office of the County Secretary and the Chairperson on Transport and Infrastructure. The first site visit was between me and Engineer Migosi from the said Department and the second site visit was between the CEO and the County Secretary and myself and indeed they have confirmed. I think that it is just the delay because of the rain but in some few days to come they promised to address the issue so am satisfied with the report from the department. Thank you.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you Hon. Bwire, yes Clerk.

RESPONSE TO STATEMENT BY CHAIRPERSON COMMITTEE ON EDUCATION ON THE LUNCH
FEEDING PROGRAM IN THE COUNTY

Yes Hon. Ibrahim Omondi.

Hon. Omondi: Thank you Mr. Speaker sir, I know most of the Members are very eager...

(Loud noise)

The Speaker (Hon. Khatri): Order Members! Please let the Hon. Member...

Hon. Omondi: Thank you Mr. Speaker for the protection that you have offered to me. Mr. Speaker sir I was saying that Members are very much eager to hear from the Department of Education on the feeding program. I was requested by Hon. Kitula and am going to be very much precise and accurate on it, Mr. Speaker sir, I want to say that we shall provide....

(Interruption)

The Speaker (Hon. Khatri): Hon. Members please order! Let the Hon. Member, if you have an issue with bursary you can stand and ask for the statement and he will reply so please let him reply on the issue he was asked.

Hon. Omondi: Mr. Speaker sir I think am answering a statement on provision of lunch to primary and high school candidates, that is exactly what am answering, not the issue of bursary, thank you. So Mr. Speaker sir I want to respond and I want to say on Sunday the Department of Education will provide or will distribute food but particularly public primary schools and the following will be given; 1 packet of milk, a bottle of water, a bread or a bun and a fruit. Mr. Speaker sir I think that this time round the education Department has done something very good and we need to be thanked. Thank you.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you. Yes Hon. Bwire.

Hon. Bwire: Thank you Mr. Speaker. Once again Mr. Speaker I want to urge this Honourable House to be serious; we are not giving much attention to the issues affecting *mwananchi*, we have been calling upon...you can hear the voices people are murmuring bursaries, no one is responding to whatever we have raised, the issue of lunch is what they have considered to be more effective and that of concern compared to the bursary. Mr. Speaker i want to urge the Department and the Committee on Education to be vigilant and serve the interest of *mwananchi*, those....

(Interruption)

The Speaker (Hon. Khatri): Hon. Bwire the statement was regarding the bursary or was it regarding the lunch?

Hon. Bwire: Of course Mr. Speaker.

The Speaker (Hon. Khatri): Who raised the statement, was it Hon. Charles Kitula?

Hon. Bwire: Of Course Mr. Speaker with your permission I understand that the statement was touching on provision of lunch to the school going children who are yet to start their final exam but we are appealing to the Members to give priority to the most issues that affect *mwananchi* than this small issue that won't give anything that will help *mwananchi* down there. Thank you.

The Speaker (Hon. Khatri): But Hon. Bwire you can appeal but not murmuring around, you can stand and ask the statement to the Hon. Member, use the procedure. Yes Hon. Charles Kitula.

Chief Whip (Hon. Kitula): Mheshimiwa nafikiri niliweza kuuliza taarifa hiyo kwa niaba ya naibu wako kwa vile alikuwa amechukua kiti chako Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ningependa kumfahamisha Mheshimiwa ambaye aliweza kuongea kwamba tatizo la kuweza kuwapatia vyakula sio shughuli ya idara ya elimu, hiyo ilikuwa ni Hassan Joho Foundation aliokuwa akitoa kila mwaka. Kwa hivyo kama ni maswala ya basari tafadhali lete kwa njia inayostahili maana yake hili ni Jumba la sheria na litajibiwa kwa njia inayostahili, kwa hivyo chakula ni Hassan Joho Foundation Mheshimiwa. Ahsante.

The Speaker (Hon. Khatri): Yes Hon. Fatma Kushe can you give Hon. Maimuna the microphone, Hon. Fatma you can use this one it's working.

Hon. (Ms.) Fatma Swaleh: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipa fursa hii, nafikiri kabla sijakosea nimemsikia kwa makini Mheshimiwa Bomoa akisema kwamba watoto maziwa, mkate na maji. Mheshimiwa Spika mimi ninavyojua safari hii naona kuna mabadiliko, maana yake Mheshimiwa Spika watoto wakitoka majumbani itakuwa wameshakunywa chai, maji watakuwa washakunywa sasa watoto siku tatu mfululizo watoto wakifanya mtihani, wakipewa maziwa na maji na mkate baada ya hapo watakuwa washafunga choo. Mheshimiwa Spika Bomoa aweze kuja na mikakati mizuri ya kutuambia kwamba watoto wetu watakula kitu gani, ahsante sana.

The Speaker (Hon. Khatri): Yes Hon. Thoya, yes Hon. Maimuna, sorry Hon. Thoya let Hon. Maimuna speak first then you.

